# SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
# WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

## FURSA ZA UFADHILI WA MASOMO NCHINI UTURUKI (TURKIYE SCHOLARSHIPS) KWA MWAKA 2026/2027.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Zanzibar inatangaza fursa za ufadhili wa masomo zilizotolewa na Serikali ya Jamhuri ya Uturuki katika ngazi za Shahada ya kwanza, Shahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamivu kwa mwaka wa masomo 2026/2027.

Ufadhili huo unajumuisha ada ya masomo, posho ya kujikimu kwa mwezi, bima ya afya, tiketi ya ndege, udahili wa chuo na usajili wa kozi (university and program placement), utafiti, malazi na mafunzo ya lugha.

Aidha taarifa zaidi kuhusu ufadhili huo ikiwemo sifa na taratibu za uombaji zinapatikana kupitia Tovuti (https://turkiyeburslari.gov.tr).

Maombi yote kuhusu ufadhili huo yanafanyika kupitia tovuti tajwa kuanzia Januari 10,2026 na mwisho wa kutuma maombi ni Februari 20,2026.

Imetolewa na:
Katibu Mkuu
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali,
S.L.P 394
Mazizini
**Zanzibar.**
**Barua Pepe:** unt.hest@moez.go.tz/hestpemba@moez.go.tz